JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 13- 2021/2022**

**DHIDI YA**

**CLOUDS TELEVISION**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI) 2018**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ilitoa leseni kwa Kituo cha **CLOUDS TELEVISION** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya Televisheni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 45 (2) na (3) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Kanuni ya 6 ya Marekebisho ya Kanuni za Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2020, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kusimamia na kufuatilia huduma za maudhui ya Redio na Televisheni ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma ye yote atakayekiuka, Maadili, Misingi na Kanuni za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni au sheria nyingine.

1.3 Tarehe 06 Juni, 2022, kati ya saa 1.00 na saa 3.00 usiku, Kituo cha Utangazaji cha **CLOUDS TELEVISION** kupitia kipindi chake cha "***Clouds E***" kinatuhumiwa kukiuka Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji kwa kutangaza maudhui yenye vionjo vya ngono/mapenzi ambayo hayafai kusikilizwa na watoto katika muda

ambao watoto wanaweza kuwa sehemu ya wasikilizaji wa vipindi vya televisheni yao.

1.4 Katika kipindi hicho, Mtangazaji wa kituo hicho alisikika akimhoji Msanii Bi. Huddah Monroes kutoka Kenya kuhusu ujio wake hapa Tanzania katika kazi zake za sanaa. Baadhi ya maneno ya mahojiano hayo ni kama ifuatavyo: -

***"...Huddah: Niliahidi ntakuja Tanzania halafu you know everyone ameniambia ulisema utakuja kutolewa nyege that's why I came for ... eee tutajua..."***

1.5 Pia, kupitia kipindi cha ***"Sentro"*** kilichorushwa tarehe 6 Juni, 2022, Kituo cha **CLOUDS TELEVISION** kinatuhumiwa kufanya mzaha wa kuweka riwaya na kibonzo cha kejeli wakati mtangazaji alipowasilisha Taarifa ya Habari kuhusu agizo la Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) la kulitaka Jeshi la Polisi kumkamata mfanyabiashara wa Mtwara aliyekuwa anatuhumiwa kuwauzia wakulima wa korosho pembejeo feki.

1.6 Baadhi ya maneno yaliyonukuliwa katika mahojiano hayo ni: -

***" Harris: Katibu mmoja wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka...***
***Msimulizi: Msake mpaka umpate ni Riwaya iliyoandikwa na Agustine Msangi ikihusu upelelezi wa kumtafuta mhalifu mmoja mtukutu mjini mhusika alikuwa bwana mmoja aitwaye Tom akiwa Afisa wa polisi alipewa jukumu la kumsaka mhalifu huyo. Ni jukumu kama hilo ndilo ambalo Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka, analitwika kwa jeshi la Polisi kumtafuta mfanyabiashara anayewauzia wakulima wa korosho pembejeo feki...Wanasema mchawi mpe mtoto akulelee aidha Shaka amefichua kuwa katika hujuma hiyo... upi mustakabali wa mfanyabiashara huyo ataingia kwenye kumi na nane za mwenezi au ndo tusubiri subiri sana; haaa he he he maan'ake kwanza hapo ncheke."***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kwa kitendo cha kutangaza na kujadili maudhui kwenye kipindi chake cha "***Clouds E***" yasiyo na staha na yenye viashiria vya ufanyaji wa ngono na yasiyofaa hasa kwa watoto na ambayo hayapaswi kutangazwa katika muda ambao watoto wanaweza kuwa sehemu ya wasikilizaji, **CLOUDS TELEVISION** inatuhumiwa kukiuka Kanuni za 11 (1) (c), 11(2) (b), 12 (1) (a), (b),(d) na 14 (a) (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018 ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

11.-(1) A licensee shall ensure that the programme and its presentation-

(c) observes good taste and decency;

(2) A licensee shall not broadcast any matter which-

(b) present sexual matters in an explicit and offensive manner;

12.-(1) A content services licensees shall-

(a) ensure that due care is exercised in order to avoid content which may disturb or be harmful to children;

(b) not broadcast programmes as referred to in paragraph (a) during family viewing of listening period;

(d) protect children from negative influences

14. Every content services licensee shall not provide content-

(a) unsuitable for children when large numbers of children may be expected to be part of the audience;

(c) which contains excessive and gross offensive language used in content transmitted during the watershed period.

Aidha, katika kipindi chake cha '***Sentro***' ambacho ni cha Taarifa ya Habari msomaji aliwasilisha taarifa hiyo kwa mzaha, kejeli na upotoshaji kwa jamii na hivyo **CLOUDS TELEVISION** inatuhumiwa kukiuka Kanuni ya 15 (2) (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018 ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

15 (2) The licensee shall: -

(c) report news in an objective and balanced manner, without intentional or negligent departure from the facts, whether by distortion, exaggeration, misrepresentation or material omission;

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

3.1 Tarehe 14 Juni 2022, Kamati ya Maudhui ilikiandikia Kituo cha **CLOUDS TELEVISION,** wito wa kuwasilisha utetezi wa maandishi na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui tarehe 22 Juni, 2022, Saa 04:00 Asubuhi ili kujieleza kwa nini hatua za kisheria zisichukuliwe dhidi yake kwa kukiuka Kanuni za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018 kama zilivyoainishwa hapo juu.

3.2 Tarehe 22 Juni, 2022, **CLOUDS TELEVISION** iliwasilisha utetezi wake wa maandishi, uliosainiwa na **Sheba Kussaga**. Pia, **CLOUDS TELEVISION**, ikiwakilishwa na **Sebastian Maganga,** Mkuu wa Maudhui; **Emilian Mallya,** Afisa Uhusiano; **Kalaghe Rashid**, Mwanasheria na **Dotto Bahemu**, Mkuu wa Vipindi walifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA MASHTAKA, KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI YA CLOUDS TELEVISION YANAYOTUHUMIWA.

4.1 Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **CLOUDS TELEVISION** mashtaka yake. Pia, Kamati na Uongozi huo kwa pamoja walisikiliza maudhui yaliyotangazwa na Kituo hicho katika tarehe na kipindi tajwa hapo juu na kisha kuwaalika kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

## 5.0 UTETEZI WA CLOUDS TELEVISION

5.1 Katika utetezi wao wa maandishi, **CLOUDS TELEVISION** walikiri kuwa maudhui yanayotuhumiwa yalitangazwa na Kituo chao. Walianza kujitetea katika kosa la kwanza la kutangaza maudhui yenye vionjo vya ngono/mapenzi na ambayo hayafai kusikilizwa na watoto katika muda ambao watoto wanaweza kuwa sehemu ya wasikilizaji. Walidai kuwa Kituo chao kilichukua hatua na kutekeleza wajibu wa kulinda walaji wake kwa kufanya uhariri ili kuondoa ukakasi wa neno lililokuwepo katika maudhui yao kama ilivyoainishwa katika Kanuni za 11 (1) (c), 11(2) (b), 12 (1) (a), (b),(d) na 14 (a) (c) za Kanuni za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018. Kwamba baada ya uhariri huo kufanyika, neno "nyege" halikusikika katika maudhui waliyoyatangaza na matamshi yaliyobaki hayakuwa na utata, hivyo kuondoa uwezekano wa mlaji wa maudhui kuelewa ni nini hasa kilizungumzwa;

5.2 Aidha, walikiri kuwa pamoja na jitihada walizofanya katika kuondoa ukakasi wa neno lililokuwepo, ni wazi kuwa bado kuna sehemu ya jamii imepata ukakasi huo. Hata hivyo, waliomba uamuzi utakaotolewa na Kamati uzingatie kuwa Kituo chao, kwa nia thabiti kilifanya jitihada za uhariri ili kuhakikisha walaji wake wanapata maudhui yaliyo safi na yasiyokinzana na Kanuni;

5.3 Pia, **CLOUDS TELEVISION** waliomba radhi kwa yeyote aliyekwazika na maudhui yao hayo na kukiri kuwa wamefanya kosa hilo bila ya kukusudia. Walisema kuwa wamekuwa wepesi wa kukiri na kuomba radhi pale wanapofanya makosa, na kwamba ni desturi yao kuheshimu, kufuata na kusimamia hatua na miongozo ya kujirekebisha inayotolewa. Waliomba kupewa adhabu nafuu kwa kadiri iwezekanavyo;

5.4 **CLOUDS TELEVISION** pia waliendelea kujitetea dhidi ya kosa la pili la kutangaza maudhui yenye mzaha, kejeli na upotoshaji kwa jamii. Walidai kuwa Kituo chao kinaheshimu Viongozi wote, na wa ngazi zote na kwa namna yoyote hawajawahi na hawana lengo la kumdhalilisha, kumdharau wala kutoa habari yenye lengo la kumkwaza Kiongozi wala kuhamasisha uchochezi wa aina yoyote ile;

5.5 Waliomba itambulike na ieleweke kwamba ili kuhakikisha wanavutia walaji zaidi, Kituo chao kinatumia mtindo wa ubunifu wa kipekee wa kuwasilisha taarifa kwa walaji, mtindo ambao unalenga kufikisha taarifa kwa njia za kibunifu, kwa lengo la kuwavutia watazamaji na kuitofautisha **CLOUDS TELEVISION** na vyombo vingine vya habari bila kuathiri Kanuni na hususani Kanuni ya 15 (2) (c) ya Kanuni tajwa za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018. Walidai kwamba Kituo chao kilitumia ubunifu ili kuipamba na kuipa upekee taarifa husika na kwa namna yoyote ile hawakuwa na lengo la kumkejeli Kiongozi au kukejeli kazi zinazofanywa katika kupambana na makosa ili kuleta maendeleo kwa Watanzania;

5.6 Waliendelea kudai kuwa riwaya iliyotajwa na kusimuliwa na Mwandishi wao, iliwekwa mahususi ili kuonesha mkazo, ukubwa na umuhimu wa maagizo aliyoyatoa Ndugu Shaka Hamdu Shaka katika kumtafuta na kumfikisha mtuhumiwa mbele ya vyombo vya Sheria;

5.7 Walimalizia utetezi wao wa maandishi kwa kuomba radhi kwa yeyote ambaye, kwa namna moja au nyingine, amekwazika na namna yao ya uwasilishaji wa taarifa. Walisema wataendeleza utamaduni wao wa kumheshimu kila mmoja na kuzipa kipaumbele habari zote zenye malengo ya kuchochea maendeleo kwa jamii kama ambavyo wamekuwa wakifanya siku zote.

Pia **CLOUDS TELEVISION** ilitoa utetezi wake kwa mdomo kama ifuatavyo:

5.8 **Sebastian Maganga** alisema kuwa "***Clouds E***" ni kipindi cha burudani na huwa wanaweka uwiano kati ya weledi na ubunifu ili kutengeneza maudhui ya kiushindani katika jamii na soko. Aliiomba Kamati izingatie kuwa Kituo chao kilifanya jitihada za kuhariri neno lililokuwa na ukakasi kwa kuwa kipindi husika kilikuwa ni cha kurekodiwa. Baada ya maswali na maelezo ya Kamati, alisema kuwa anatambua lengo la Kamati ni kuwaongezea weledi na maarifa na wameyapokea yote hayo kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Aliendelea kusema kuwa wanatamani kuwa na utofauti kwenye soko ila wanatambua kuwa wanapaswa kuzingatia vigezo, viwango na misingi ya taaluma ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Kwamba, dhamira yao ni njema ila wataboresha zaidi ili wasikiuke misingi inayokubalika. Alisema haikuwa dhamira ya mwandishi wao kutomtaja Ndugu Shaka Hamdu Shaka ila kilichotokea ni kuteleza tu. Alisema kibonzo walichokiweka kwenye taarifa yao, "haaa he he he maan'ake hapo kwanza ncheke" kinaweza kuleta tafsiri tofauti na hivyo uwasilishaji wa ubunifu wao haukuwa sahihi.

5.9 **Kalaghe Rashid** aliiomba Kamati izingatie hatua zilizochukuliwa na Kituo chao za kuhariri maudhui yanayotuhumiwa ili kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Kanuni ya 12(1)(a) ya Kanuni za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018.

5.10 **Dotto Bahemu** alieleza kuwa kwa namna neno lenye ukakasi lilivyosikika, inaonesha wazi kuwa walifanya jitihada za kulihariri. Alisema kuwa wanatambua cheo cha Ndugu Shaka Hamdu Shaka, hawakuwa na dhamira ovu na wametambua kuwa uwasilishaji wa ubunifu wao haukuwa sahihi, na hivyo wanatakiwa kuwa na ubunifu wenye tija na usiokiuka misingi ya taaluma.

5.11 **Emilian Mallya** alisema kuwa wamepokea na kujifunza mengi kupitia maswali na maelezo ya Kamati na watayafanyia kazi. Alisema kuwa wametambua kuwa wamekosea ila hawakudhamiria bali dhamira yao njema ilitofautiana na ubunifu wao. Alisema wanafahamu umuhimu na ukubwa wa Viongozi wa Chama na Serikali. Alisema pia kuwa wameona umuhimu wa kuendelea kuwajengea uwezo Waandishi wao ili kuboresha maudhui yao. Alimalizia kwa kuomba radhi.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imezingatia maelezo yote ya **CLOUDS TELEVISION** na kubaini kuwa Kituo kimetenda kwa uzembe, kosa la kutangaza maudhui yasiyo na staha, yenye lugha ya matusi yenye kuashiria ufanyaji wa ngono/mapenzi na yasiyofaa hasa kwa watoto na ambayo hayapaswi kutangazwa katika muda ambao watoto wanaweza kuwa sehemu ya watazamaji, kama walivyokiri wenyewe na kama ambavyo neno lenye ukakasi "nyege" limesikika katika maudhui yao yaliyotuhumiwa. Kitendo hiki ni kinyume na Kanuni za 11 (1) (c), 11(2) (b), 12 (1) (a), (b), (d) na 14 (a) (c) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018;

Kamati imebaini na kuzingatia kuwa CLOUDS TELEVISION walifanya jitihada za kiuhariri kutolifanya neno Nyege lisisikike kikamilifu. Hata hivyo, neno hilo lilisikika na ujumbe uliokusudiwa ulifika na kueleweka vizuri kwa watazamaji wake. Hivyo Kamati imeona kuwa utetezi wa **CLOUDS TELEVISION** kuwa walifanya jitihada za kuhariri neno lililokuwa na ukakasi hauna msingi wowote kwa sababu imeonekana wazi kuwa neno hilo lilisikika na kueleweka kwa watazamaji wao, kama ambavyo wamekiri wenyewe pia. Kwa kuwa maudhui hayo yalikuwa ni ya kurekodiwa, **CLOUDS TELEVISION** walikuwa na nafasi ya kutotumia maudhui hayo yasiyokuwa na staha.

6.2 Pia, Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **CLOUDS TELEVISION** ilikosa usimamizi/uhariri makini na hivyo kuruhusu maudhui hasi na yasiyo na staha kutangazwa hewani katika muda ambao watoto wanaweza kuwa sehemu ya watazamaji. Maudhui yaliyorushwa hewani yalikosa weledi na maadili na yanaweza kuchochea mmonyoko wa maadili kwa watoto. **CLOUDS TELEVISION,** kama chombo cha habari ina wajibu wa kuilinda jamii dhidi ya maudhui yasiyokuwa na staha na kuhakikisha kuwa utamaduni na maadili ya jamii ya Kitanzania yanatunzwa.

6.3 Kamati imebaini kuwa **CLOUDS TELEVISION** imetenda kwa uzembe, kosa la kutangaza na kujadili maudhui yenye mzaha, kejeli na upotoshaji kwa jamii na katika kipindi cha Taarifa ya Habari kinyume na Kanuni ya 15 (2) (c) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018. Mtangazaji wa **CLOUDS TELEVISION** alitenda kosa hili kwa kuweka kibonzo cha kejeli/mzaha cha ***"haaa he he he maan'ake kwanza hapo ncheke"*** wakati akitangaza Taarifa ya Habari iliyomuhusu kiongozi huyo wa Chama Cha Mapinduzi.

6.4 Kamati imeona kuwa madai ya **CLOUDS TELEVISION** kuwa walifanya ubunifu katika taarifa yao ya Habari hayana msingi wowote kwa sababu ubunifu wanaodai kuufanya haukuwa sahihi, hivyo uliwapelekea kukiuka Kanuni, Weledi na Misingi ya taaluma ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Kamati imebaini kuwa ubunifu wanaodai kuufanya, haukuwa na tija wala manufaa, bali ulikiuka Kanuni na Misingi ya utangazaji wa kipindi cha Taarifa ya Habari na hivyo kuishushia hadhi Taarifa yao ya Habari. Pia, ubunifu wanaodai kuufanya hauendani na Misingi ya Utangazaji wala utaratibu na ubora unaokubalika wa uwasilishaji wa Taarifa za Habari (Best Practice).

6.5 Kamati imegundua kuwa **CLOUDS TELEVISION** wana mapungufu katika maandalizi/utayarishaji na usimamizi wa vipindi vyao, jambo lililowapelekea kutenda makosa tajwa.

## 7.0 MAELEKEZO YA KAMATI KWA CLOUDS TELEVISION

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inatoa maelekezo yafuatayo kwa **CLOUDS TELEVISION**: -

7.1 Kuhakikisha inazingatia Misingi, Sheria, Kanuni, Maadili, Weledi, Vigezo na Viwango vya tasnia ya Uandishi na Utangazaji wa Habari katika kutayarisha/kuandaa, kusimamia na kutangaza vipindi vya Taarifa za Habari na maudhui yao kwa ujumla;

7.2 Kuhakikisha inazingatia ubunifu sahihi wenye tija, manufaa, uwajibikaji na unaoendana na misingi inayokubalika katika uwasilishaji wa maudhui;

7.3 Kuhakikisha inazingatia utaratibu na ubora unaokubalika wa uwasilishaji wa Taarifa za Habari (Best Practice);

7.4 Kuzingatia maandalizi na usimamizi makini wa vipindi vyao;

7.5 Kuhakikisha kuwa wanatumia lugha fasaha na yenye staha katika uwasilishaji wa maudhui yao.

7.6 Kuhakikisha inaendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma waandishi/watangazaji wao ili wawe na ubunifu wenye tija katika kazi zao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

8.1 Baada ya kutafakari kwa kina utetezi uliowasilishwa na **CLOUDS TELEVISION**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **CLOUDS TELEVISION** imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018 kama ilivyoainishwa katika Tathmini ya Kamati hapo juu.

8.2 Hivyo basi, kwa mujibu wa Kifungu cha 44 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano, Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017 pamoja na Kanuni ya 45 (2) na (3) (a) ya Kanuni tajwa za Utangazaji wa Maudhui ya Redio na Televisheni, 2018 kama ilivyofanyiwa marekebisho ya Kanuni ya 6 ya Marekebisho ya Mwaka 2020, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu ifuatayo kwa **CLOUDS TELEVISION:**

1. Inapewa Onyo kwa makosa yote mawili yaliyobainishwa hapo juu.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **01 Julai, 2022**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Ndalahwa Habbi Gunze**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

................................................................................
**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Derek Kaitira Murusuri** ....................................
2. **Jacob Gregory Tesha** ....................................